

# 新编斯瓦希里语 2

# KISWAHILI
## Kitabu cha Pili

曹 勤 孙宝华 冯玉培 编著



外语教学与研究出版社

# 新编
# 斯瓦希里语 2

## KISWAHILI
## Kitabu cha Kwanza

曹 勤 孙宝华 冯玉培 编著

外语教学与研究出版社

北京

图书在版编目(CIP)数据

新编斯瓦希里语. 第2册/曹勤, 孙宝华, 冯玉培编著 .— 北京: 外语教学与研究出版社, 2008.2
ISBN 978-7-5600-7272-2

Ⅰ. 新… Ⅱ. ①曹… ②孙… ③冯… Ⅲ. 斯瓦希里语—高等学校—教材 Ⅳ. H823

中国版本图书馆 CIP 数据核字 (2008) 第 024823 号

出 版 人: 于春迟
责任编辑: 孙纪晓
封面设计: 袁 璐
出版发行: 外语教学与研究出版社
社 址: 北京市西三环北路 19 号 (100089)
网 址: http://www.fltrp.com
印 刷: 北京外国语大学印刷厂
开 本: 850×1168 1/32
印 张: 11.125
版 次: 2008 年 3 月第 1 版 2008 年 6 月第 2 次印刷
书 号: ISBN 978-7-5600-7272-2
定 价: 20.00 元
* * *
**如有印刷、装订质量问题出版社负责调换**
**制售盗版必究 举报查实奖励**
**版权保护办公室举报电话: (010)88817519**
**物料号: 172720001**

# 前　　言

本书为斯瓦希里语教科书第二册，供斯语基础阶段教学使用。

本册书共教授斯语词汇 950 个左右。讲授的基本语法为 u，pa，ku 三类名词、某些常用的动词时态（ki，ka，a，sipo 等）、动词主要派生形式（被动式，相互式，趋为式，状态式，使役式、反义式等）以及关联词素-o-和 amba 的用法。

练习部分，根据当前外语考试标准化试题的要求，我们增加了多种类型的选择填空及阅读理解等能力测试项目。此外，每课书后都附有两条常用斯语谚语，以提高学生的语言水平和学习兴趣。

编　者

2007 年 11 月

# YALIYOMO

Somo la Kwanza……………………………………………………1

Somo A: Urafiki wa Dhati

Somo B: Baada ya Siku za Mapumziko

Sarufi: Wakati wa "ki"

Somo la Pili……………………………………………………15

Somo A: Kumtembelea Rafiki wa Tanzania

Somo B: Magazeti ya Tanzania

Sarufi: Wakati wa "sipo" na "A"

Somo la Tatu……………………………………………………32

Somo A: Jua na Upepo

Somo B: Maji na Moto

Sarufi: Ngeli ya U; wakati wa "hu"

Somo la Nne……………………………………………………48

Somo A: Kusafiri kwa Basi

Somo B: Safari ya Basi

Sarufi: Hali ya Kutendeana

Somo la Tano……………………………………………………64

Somo A: kumpokea Mgeni

Somo B: Kumsindikiza Mgeni

Sarufi: Hali ya kutendea



此为试读，需要完整PDF请访问：www.ertongbook.com

Somo la Sita ........................................................ 79

Somo A: Dukani

Somo B: Kwenda Dukani

Sarufi: Hali ya Kutendwa

Somo la Saba ........................................................ 97

Somo A: Mashujaa wa Tanzania

Somo B: Julius Nyerere Mzalendo Halisi

Sarufi: Vitenzi Vyenye Silabi Moja

Somo la Nane ........................................................ 113

Somo A: Mazungumzo Juu ya Hali ya Hewa

Somo B: Utabiri wa Hali ya Hewa

Sarufi: Ngeli ya "pa" na "ku"

Somo la Tisa ........................................................ 128

Somo A: Mashindano ya Mbio Kati ya Sungura na Kobe

Somo B: Mbweha na Kobe Wagombea Utemi

Sarufi: Wakati wa "ka"

Somo la Kumi ........................................................ 144

Somo la Marudio

Bwana Tungkuo na Mbwa Mwitu

Somo la Kumi na Moja ........................................................ 158

Somo A: Nchi Yetu

Somo B: Beijing

Sarufi: Matumizi ya -enye,-enyewe na -pi

Somo la Kumi na Mbili··········175

Somo A: Habari Fupi Juu ya Tanzania

Somo B: "Mama Misitu" Apata Tuzo la Nobel

Sarufi: Tarakimu

Somo la Kumi na Tatu··········192

Somo A: Kutembelea Ukuta Mkuu

Somo B: Masalia ya Historia ya Tanzania

Sarufi: Asilimia, Sehemu (fraction), Desimali (decimal)

Somo la Kumi na Nne··········209

Somo A: Esopo

Somo B: Androkleo

Sarufi: Kirejeshi - o -

Somo la Kumi na Tano··········225

Somo A: Nani Bora

Somo B: Umoja ni Nguvu

Sarufi: amba

Somo la Kumi na Sita··········241

Somo A: Kasri ya Majira ya Joto

Somo B: Maonyesho ya Sanaa za Tanzania

Sarufi: Hali ya Kutendeka

Somo la Kumi na Saba··········258

Somo A: Kupambana na Maadui Watatu

Somo B: Sikukuu ya Uhuru na Jamhuri

Sarufi : Hali ya kutendesha

Somo la Kumi na Nane··········278

Somo A: Mtaka cha Mvunguni Sharti Ainame

Somo B: Asiyesikia la Mkuu Huvunjika Guu

Sarufi : Vitenzi Vyenye Maana ya Kinyume

Somo la Kumi na Tisa··········295

Somo A: Wakenya Wanaitakidi Nini?

Somo B: Bendera ya Taifa ya Kenya

Sarufi: Matumizi ya Vivumishi

Somo la Ishirini··········315

Somo la Marudio

Mila na Utamaduni wa Zanzibar

Orodha ya Msamiati··········327

# SOMO LA KWANZA

| | |
|---|---|
| Somo A: | Urafiki wa Dhati |
| Somo B: | Baada ya Siku za Mapumziko |
| Sarufi: | Wakati wa "ki" |

MAZUNGUMZO

(1)

A: Je, ukimaliza masomo yako utafanya kazi gani?

B: Nikimaliza masomo yangu nitafanya kazi ya ufundi.

A: Wapi utafanya kazi hiyo?

B: Nitafanya kazi hiyo huko Dar es Salaam.

A: Ukienda Dar es Salaam utakaa wapi?

B: Nikienda Dar es Salaam nitakaa katika sehemu ya Mnazi Mmoja.

A: Ukiwa huko utashughulika na nini?

B: Nikiwa huko nitashughulika na kazi ya kutengeneza mashine.

A: Je, ukipata likizo utarudi hapa Unguja?

B: Ndiyo. Nikipata likizo nitarudi hapa Unguja.

MAZUNGUMZO

(2)

Haji: Mwalimu, tukimaliza mtihani bora twende kupanda mlima Jumapili hii, wasemaje?

Mwal: Shauri zuri. Nilipokuwa kijana kama ninyi nilipanda milima mara

kwa mara.

Haji: Kama tukipanda mlima mrefu tutaweza kuona mandhari nzuri ya nchi yetu.

Mwal: Tena msisahau kuwa tukipanda mlima mara kwa mara itatusaidia kujenga afya zetu.

Haji: Haya bora twende Jumapili hii, lakini ikinyesha mvua hatutakwenda, sivyo?

Mwal: Ndivyo. Ikinyesha mvua tutakwenda siku nyingine.

MAZUNGUMZO

(3)

Hang: Nimesikia kuwa Tanzania na Kenya ni nchi zenye mandhari ya kuvutia, ni kweli?

Mwal: Ni kweli. Ukienda sehemu ya pwani utaweza kuona fukwe nzuri za bahari.

Hang: Nikienda Bara nitaweza kuona mandhari ya kuvutia vilevile?

Mwal: Ndiyo. Ukienda Bara utaona milima, mito, maziwa na miti ya maua hapa na pale. Ukienda huko Moshi utaona mlima mrefu kabisa katika Bara la Afrika yaani Mlima Kilimanjaro.

Hang: Hata katika kitabu cha jiografia nilipata kusoma kuwa katika kilele cha Mlima Kilimanjaro kuna theluji mwaka mzima.

Mwal: Huu ni ukweli mtupu. Ndiyo maana kila mwaka watalii wengi wanakwenda kuupanda mlima huo maarufu.

Hang: Nikipata nafasi nitatembelea nchi hizi za Afrika ya Mashariki.

Mwal: Ukifika Tanzania au Kenya wenyeji wa huko watakukaribisha

kwa mikono miwili.

## MAZUNGUMZO
## (4)

Mwal: Leo ni Jumapili, je, wanafunzi wa darasa lenu wanafanya nini?

Ling: Mkuu wa darasa letu na Ndugu Wang wanatembea uwanjani huku wakizungumza Kiswahili.

Mwal: Je, wasichana wanafanya nini?

Ling: Wasichana wanafua nguo huku wakiimba kwa furaha.

Mwal: Na wavulana wengine wanafua nguo vilevile?

Ling: Hapana. Wanasikiliza idhaa ya Kiswahili huku wakiandika misamiati.

Mwal: Je, Jumapili mnafanya kazi za nyumbani?

Ling: Ndiyo. Na baada ya kumaliza kazi za nyumbani kila mtu anafanya shughuli zake kama anavyopenda.

## SOMO A
## URAFIKI WA DHATI

Siku moja saa nane hivi alasiri, baharia mmoja kutoka Uingereza alizunguka na kuhangaika huku na huko kwenye bandari ya Kanton huku akikunja uso na kuvuta sigara kwa nguvu.

Wakati huo alitokea mfanyakazi mmoja wa bandarini. Vitendo vya yule mgeni vilimshangaza sana. Alisimama huku akijiuliza: "Kwa nini yule mgeni anahangaika namna ile? Ana shida gani?" Bila ya kujizuia



此为试读，需要完整PDF请访问：www.ertongbook.com

alimwendea yule mgeni na kumwuliza kwa upole, "Hujambo rafiki! Je, unatafuta nini hapa? Au umepoteza kitu?" Kusikia vile, yule mgeni alimwambia, "Mimi sijambo, asante. Sina shida kubwa isipokuwa saa yangu ya mkononi imetumbukia majini, na mimi sina njia ya kuipata tena. Unajua saa hii nilipewa na rafiki yangu, nikiipoteza basi nitamweleza nini baada ya kurudi nchini kwetu? Ah! Balaa hilo!"

Baada ya kuyasikia maneno yake, mfanyakazi yule alimwambia, "Rafiki yangu, usiwe na wasiwasi, nitafanya maarifa ya kuipata saa yako!" Alisema huku akivua nguo zake. Halafu alitumbukia majini na kupiga mbizi. Dakika nzima ilipita yule bwana hakuibuka. Yule mgeni alianza kuwa na wasiwasi. Dakika nyingine baadaye yule mfanyakazi aliibuka na saa mkononi. Kisha aliogelea mpaka kwenye ngazi za gati na kupanda juu. Yule mgeni alipoipokea saa yake alishindwa kusema mengi, aliyarudia tena na tena maneno haya, "Nakushukuru sana! Nakushukuru sana!" Yule mfanyakazi alimwambia, "Usiseme maneno haya. Ni wajibu wangu kufanya hivyo. Nafurahi sana kuwasaidia marafiki zetu."

Baada ya kusikia maneno haya, yule mgeni alisema, "Sina budi kutoa shukurani zangu nyingi kwako wewe, na kwa watu wa China. Sisi ni marafiki wema."

Kweli, kitendo hiki cha yule mfanyakazi wa bandarini kimeonyesha moyo safi na urafiki wa dhati wa watu wa China kwa watu wa dunia nzima.

## MSAMIATI

| | |
|---|---|
| likizo (n) 假日，假期 | pwani (n) 海边，沿海地带 |
| mtihani (mi) 考试，考核，考验 | ufukwe (u) 海滩，沙滩 |

mlima ( mi ) 山
mto (mi) 河，河流
kilele (ki) 山顶，顶峰
theluji (n) 雪
ukweli (u) 真理，事实
-tupu (kv) 空的，单一的
-tembea (kt) 散步，走路
furaha (n) 高兴，快乐
dhati (n) 真诚
baharia (wa) 海员，水手
-zunguka (kt) 转圈
Uingereza (n) 英国
bandari (n) 港口
-kunja (kt) 折叠，皱起
-vuta (kt) 吸，拉
sigara (n) 香烟
nguvu (n) 力量，力气
-tokea (kt ) 出现，发生
kitendo (ki) 动作，行为
-shangaza (kt) 使……惊奇
-zuia (kt) 阻止
-jizuia (kt) 抑制自己
upole (u) 和蔼
-poteza (kt) 丢失，失去
isipokuwa (kl) 除了，除……外，只是
-tumbukia (kt) 跳进，掉进
maji (ma) 水
-pewa (kt) 被授予，得到
balaa (ma) 灾难，不幸
maarifa (ma) 经验，办法
-vua (kt) 脱（衣服、鞋、帽子）
-piga mbizi (kt) 潜水，俯冲
-pita (kt) 经过，路过
kisha (kl) 然后
-ibuka (kt) 冒出，浮起
ngazi (n) 梯子，阶梯
gati (ma) 码头
-shindwa (kt) 失败，不能
-shukuru (kt) 感谢，谢谢
wajibu (u) 责任，义务
sina budi 我必须，我应该
shukurani (n) 感谢，谢意
Moshi 莫希
Kilimanjaro 乞立马扎罗

# MAELEZO YA SARUFI

## 动词-ki-时态的用法

I. -ki-时态表示“如果”、“假如”等意思，用在条件句中，后面主句中的动词一般多用将来时。

k.m. 1. Mwaka huu zikinyesha mvua za kutosha mavuno yatakuwa mazuri.

2. Nikivuta sigara nyingi, usiku nitakohoa sana.

3. Ukija kwangu nitakueleza mambo yote, na bila shaka utafurahi sana.

II. 和 huku 一起使用，表示同时发生的两个动作。

k.m. 1. Wanatembea uwanjani huku wakizungumza.

2. Wanacheza dansi huku wakiimba.

3. Wasichana wale wanateleza juu ya barafu huku wakiongea kwa furaha.

## SOMO B

## BAADA YA SIKU ZA MAPUMZIKO

A: Tazama, Ndugu C amerudi, hebu twende upesi tukamsaidie kuchukua mizigo.

B: Haya, twende.

A na B： Hujambo Ndugu C! Habari za mapumziko?

C: Ohoo njema, asante. Na habari za hapa chuoni?

A: Nzuri tu. Hebu nipe sanduku lako nikusaidie.

B: Na nipe huu mkoba wako.

C: Asanteni sana kwa wema wenu.

A: Je, umefika stesheni ya Beijing saa ngapi? Kwa nini hukutuarifu kwa simu ili tuweze kuja kukupokea?

C: Nilifika stesheni kama saa moja hivi. Kwa vile sina mizigo mingi, na mimi mwenyewe naweza kuichukua. Kwa hivyo sikutaka kukusumbueni.

B: Ehee, ulipitisha vipi siku zako za mapumziko? Naona umenenepa kidogo.

C: Kweli? Labda nilikula sana nilipokuwa nyumbani, ndiyo maana nimenenepa.

A: Ulifanya nini katika siku za mapumziko?

C: Nilisoma vitabu vingi vya hadithi; nilikwenda kuwatembelea marafiki zangu wa shule ya sekondari, tena niliwasaidia wazee wangu kufanya kazi mbalimbali. Kwa jumla nilipitisha siku za mapumziko kwa furaha sana.

B: Hebu tueleze kidogo hali ya hivi sasa ya mashambani!

C: Ohoo hivi sasa hali ya mashambani ni nzuri sana. Mwaka jana mavuno yalikuwa mazuri. Nilipokwenda vijijini kuwatembelea marafiki zangu niliona kazi za kila aina zinaendelea motomoto. Wakulima wanafurahia sana maisha mazuri ya kisasa.

A: Inafurahisha sana. Hali ya kilimo ya nchi yetu inakuwa nzuri mwaka baada ya mwaka.

C: Je, habari za hapa chuoni? Nyote mlipitisha vizuri siku za mapumziko?

B: Ndiyo, tulisoma vitabu vingi, ama vya Kiswahili au vya Kiingereza. Alasiri kwa kawaida sisi tunapenda kusoma magazeti kidogo, halafu kucheza michezo ya aina mbalimbali.

A: Na wengine wanapenda kutembea kwenye mtandao, au kuchezea michezo ya kompyuta.

C: Je, kulikuwa na sherehe yoyote hapa chuoni?

B: Hapana, lakini tulitazama filamu nyingi, na pia tulikwenda kutembelea Ukuta Mkuu.

C: Inaonyesha sote tulipitisha kwa furaha siku za mapumziko, na sasa masomo yameanza tena, lazima tujitahidi zaidi ili tuweze kupata maendeleo katika muhula mpya.

A na B: Sawa kabisa.

## MSAMIATI

mapumziko (ma) 休息

mkoba (mi) 手提包

-sumbua (kt) 打扰，使……厌烦

-pitisha (kt) 度过，通过

-nenepa (kt) 长胖，发福

vuno (ma) 收割，收获

moto (mi) 火

kilimo (ki) 农业

ama … au … 或者……或者……

sherehe (n) 仪式，庆典

Ukuta Mkuu 长城

**METHALI ZA KISWAHILI**

Kweli ikidhihiri uwongo hujitenga.

事实胜于雄辩。

Ukijua kupata ujue na kukosa.

有得必有失。

## MAZOEZI

I. Ufahamu:

A

1. Hadithi hii ilitokea wakati gani na mahali gani?
2. Kitu gani kilimshangaza sana yule mfanyakazi wa bandarini?
3. Baharia wa Uingereza alimjibu vipi mfanyakazi wa bandarini?
4. Yule mgeni alisema nini kuhusu saa yake ya mkono?
5. Baada ya kuyasikia maneno ya yule mgeni, mfanyakazi wa bandarini alimwambia nini? Na alifanya nini?
6. Yule mgeni alikuwaje alipoipokea saa yake?
7. Kwa kusikia maneno ya mgeni yule mfanyakazi alimwambia nini?
8. Kitendo cha mfanyakazi wa China kimeonyesha nini?
9. Eleza hadithi hii kwa maneno yako mwenyewe.

B

1. Kwa nini ndugu C hakuwapigia simu marafiki zake A na B ili waweze kwenda stesheni kumpokea?
2. Tafadhali eleza jinsi ndugu C alivyopitisha likizo yake na aliona nini wakati wa likizo huko vijijini?
3. Je, ndugu A na B wakati wa likizo pia walirudi nyumbani?
4. Ndugu A na B walifanya nini katika siku za mapumziko?
5. Na wewe ulipitisha vipi siku zako za mapumziko?

II. Kamilisha sentensi hizi ukitumia nyakati zinazofaa:

1. Wewe ......(-lala) sana......(-chelewa) darasani.



此为试读，需要完整PDF请访问： www.ertongbook.com